

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI

Anwani ya Simu: “Uvuvi”
Simu Nambari: +255 (026) 2322612
Nukushi: +255 (026) 2322613
Barua pepe: ps@uvuvi.go.tz
Tovuti: <http://www.mifugouvuvi.go.tz>



Mji wa Serikali Mtumba,
Mtaa wa Ulinzi,
S.L.P 2847,
40487 DODOMA

14 Februari, 2024

TAARIFA KWA UMMA

**USAJILI WA VYOMBO VYA UVUVI NA UKATAJI WA LESENI ZA VYOMBO
VYA UVUVI KWA MWAKA 2024**

Wizara ya Mifugo na Uvuvi, inapenda kuwatangazia wananchi wote wanaojishughulisha na uvuvi kwamba, msimu wa kukata leseni za vyombo vya uvuvi umeanza **tangu Januari 1, 2024**. Kwa mujibu wa Kanuni za Uvuvi za Mwaka 2009; Kanuni Na. 3 (1-4), Kanuni 4 (1-6) na Kanuni 13 (1) chombo chochote kinachojihusisha na shughuli za uvuvi ni lazima kiwe kimesajiliwa na kukatiwa leseni.

Aidha, kwa mujibu wa Kanuni za Uvuvi za Mwaka 2009, Kanuni 7(3) na (4), Chombo kilichopatiwa hati ya usajili na kupewa namba, inatakiwa namba hiyo iandikwe katika ubavu pande zote mbili za chombo. Kanuni ya 7 (1-5) na Jedwali la 3 inatoa mwongozo wa uandishi wa namba za usajili zinavyotakiwa kuwekwa katika chombo.

Zoezi la usajili na utoaji wa leseni za uvuvi **litaisha tarehe 31 Machi, 2024**, baada ya hapo wamiliki wa vyombo vya uvuvi watakaobainika kuwa hawajasajili vyombo vyao wala kukata leseni za uvuvi watachukuliwa hatua za kisheria ikiwemo kulipa faini kwa mujibu wa Sheria ya Uvuvi. Taratibu za usajili wa vyombo na Leseni za uvuvi zinapatikana katika tovuti ya Wizara (<https://www.mifugouvuvi.go.tz>), Ofisi za Kanda za Wizara na Halmashauri zote zenye shughuli uvuvi nchini.

Imetolewa na;

Prof. Riziki S. Shemdoe
KATIBU MKUU
WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI